



**Kuwa Tayari.
Kaa Umekingwa.**

Seti za Zana ya Mawasiliano ya Kidijitali

Kila mwaka, Jimbo hukagua taarifa za wanachama wa Medicaid ili kuhakikisha kuwa bado wanastahiki huduma hiyo. Kama sauti inayoaminika katika jumuiya yako, unaweza kuwahimiza wakazi wa Rhode Island wanaostahiki kuchukua hatua zinazowasaidia kuendelea kuhudumiwa na Medicaid. Katika seti hii ya zana, utapata sampuli za machapisho ya mitandao ya kijamii na blabu wa kijarida ili kueneza ufahamu kuhusu ufanyaji upya wa Medicaid. Tafsiri na nyenzo zinapatikana kwenye staycovered.ri.gov/education-materials.

Tafadhali zingatia kushiriki ujumbe huu na mtandao wako. Asante.



**KUWA TAYARI.
KAA UMEKINGWA.**

Je, Umekingwa na Medicaid?

Unachohitaji kujua kuhusu kufanya upya huduma yako ya afya.

Kila mwaka, Jimbo hukagua taarifa za wanachama wa Medicaid ili kuhakikisha kuwa bado wanastahiki. Ikiwa tuna maelezo ya kutosha, tutakutumia notisi (Notisi ya Uamuzi wa Faida) kukuambia kwamba tumefanya upya Medicaid yako.

Ikiwa tunahitaji maelezo zaidi, **tutakutumia notisi mbili:**

- 1 Notisi ya manjano ya kufanya upya Medicaid.
- 2 Notisi nyeupe inayoomba hati za ziada.

Notisi hizi mbili zitatumwa kwa barua za posta tofauti. Hakikisha unangoja zote mbili.

Mambo 3 unayoweza kufanya ili kuwa tayari na kuendelea kuingwa.

1. **Sasisha maelezo ya akaunti yako** ili Jimbo liweze kukufikia na taarifa muhimu. Kwa mfano, unapaswa kusasisha akaunti yako ikiwa maelezo yako ya mawasiliano yamebadilika, umepata kazi mpya au umepata mtoto.
2. **Ngoja barua kutoka Jimbo la Rhode Island.** Ikiwa mpango wa Medicaid unahitaji maelezo zaidi ili kufanya upya huduma yako, utapata notisi ya njano. Pia utapata notisi nyeupe inayouliza hati za ziada. Vinginevyo, utapata notisi inayosema kwamba huduma yako imeendelea kiotomatiki.
3. **Chukua hatua mara moja. Ukipata notisi ya njano,** inamaanisha kuwa Jimbo linahitaji maelezo zaidi kukuhusu wewe au watu wa kaya yako ili kufanya upya huduma yako. Tafadhali wasilisha taarifa zote zilizoombwa kabla ya tarehe ya mwisho kwenye taarifa yako.

Una maswali?

Usaidizi unapatikana. Piga Simu:

- HealthSource RI 1.855.840.4774
- RI Idara ya Huduma za Binadamu 1.855.697.4347

Dhibiti akaunti yako mtandaoni:

Enda kwa healthyrhode.ri.gov au kwa kutumia programu ya simu ya HealthyRhode. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu kufanya upya Medicaid au kuangalia wakati kufanya upya kwako kutafanyika, tembelea staycovered.ri.gov.

MITANDAO WA KIJAMII

RI Medicaid inataka kuhakikisha kuwa wewe na familia yako mnapata taarifa muhimu kuhusu bima yako ya afya. Hakikisha kuwa anwani yako imesasishwa na kwamba unasoma kila kitu unachopokea kupitia barua ya posta kutoka Jimbo la Rhode Island au shirika lako la Usimamizi wa Huduma. Ili kujifunza zaidi, tembelea staycovered.ri.gov.

Ukipata bima ya afya kupitia Medicaid, utapata notisi kupitia barua ya posta kutoka Jimbo la Rhode Island kuhusu kufanya upya huduma yako kila mwaka. Ili kuangalia tarehe yako ya kufanya upya, tembelea staycovered.ri.gov.

Ikiwa familia yako ina bima ya afya kupitia Medicaid, utapata notisi kwenye barua ya posta kuhusu kufanya upya huduma yako kila mwaka. Kwa habari zaidi katika lugha nyingi, tembelea staycovered.ri.gov.

Wanachama wa Medicaid! Je, umekuwa na mabadiliko katika anwani, mapato, ukubwa wa kaya, nambari ya simu au barua pepe? Unaweza kusasisha maelezo yako wakati wowote kwa kutembelea healthyrhode.ri.gov



Je, umekingwa na Medicaid?

Pata maelezo muhimu kuhusu bima ya afya ya familia yako.






Je, umekingwa na Medicaid?


Pata maelezo kuhusu kufanya upya huduma yako kwenye staycovered.ri.gov






Je, umekingwa na Medicaid?

Jitayarisha kufanya upya huduma yako kila mwaka. Weka taarifa yako ya mawasiliano ikiwa imesasishwa.





Je, umekingwa na Medicaid?

Utapata notisi katika barua ya posta wakati ni zamu yako ya kufanya upya.

